# KUKUBALIWA KATIKA HOSPITALI KWA MATIBABU

(Sehemu ya 3 ya Sheria ya Afya ya Akili 1983)

| | |
|---|---|
| 1. Jina la Mgonjwa: | |
| 2. Jina la mtu anayekutunza (“daktari wako aneyewajibika’) | |
| 3. Jina la hospitali na wadi | |
| 4. Tarehe ambayo kuzuiliwa kulianza chini ya sehemu ya 3 | |

## Je! ni kwanini niko hospitalini?

Unawekwa hospitalini chini ya sehemu ya 3 ya Sheria ya Afya ya Akili1983. Hii inamaanisha kuwa madaktari wawili wanafikiria kuwa unayo shida ya akili na unahitaji kuwa hospitalini ili uweze kupewa matibabu na utunzaji.

## Je! nitakuwa hapa kwa muda gani?

Unaweza kuwekwa hapa kwa muda wa hadi miezi sita kwa mara ya kwanza ili uweze kupewa matibabu unayohitaji.

Usitoke hapa wakati huo isipokuwa mtu anayesimamia utunzaji wako ( daktari wako anayewajibika) akuambie unawezatoka. Ukijaribu kutoka, wafanyikazi wanaweza kukuzuia, na ikiwa utatoka, unaweza kurudishwa.

## Je! ni nini hufanyika baadaye?

Daktari wako anayewajibika atakuambia wanapofikiria umepona ya kutosha wewe kutoka hospitalini. Ikiwa daktari wako anayewajibika anafikiria kuwa unahitaji kukaa hospitalini kwa muda unaozidi miezi sita, wanaweza kubadilisha ni muda gani unaweza kuwekwa hospitalini kwa miezi sita zaidi, kisha hadi mwaka moja kwa wakati mmoja. Daktari wako anayewajibika atazungumza nawe kuhusu haya ukielekea mwisho wa kipindi hicho.

